UTEKELEZAJI WA VIKWAZO VYA UMOJA WA MATAIFA NA MAMLAKA ZA KUDHIBITI MIPAKA

1. Utangulizi

Utekelezaji wa Vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa unahitaji nia nzuri kutoka kwa nchi wanachama na ufanisi na kuwa tayari kwa taasisi anuwai miongoni mwa Nchi Wanachama za Umoja wa Mataifa.

Mojawapo kati ya taasisi muhimu ni usimamizi wa Mamlaka za Ushuru uliopewa vifaa vinavyohitajika na pia unaoungwa mkono. Mamlaka za Ushuru zinafanya shughuli muhimu kama safu ya kwanza ya ulinzi kuhusiana na kudhibiti yale yanayoingia nchini. Vivyo hivyo, pia ni safu ya mwisho ya ulinzi pale bidhaa zinapotoka nchi fulani. Ili kuweza kufanya hivi kwa ufanisi, sheria zinazohitajika kuunda mpangilio wa kisheria zinahitaji kuundwa. Hii haihusishi tu bidhaa za nchi zilizowekewa Vikwazo vya Umoja wa Mataifa, ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DPRK), lakini pia bidhaa zote chini ya udhibiti wa Mamlaka yake ya Ushuru. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) imebuni sheria sawia za mamlaka za ushuru ambazo zinadhibiti mtiririko wa bidhaa kuelekea na kutoka nchini, kwa mujibu wa maafikiano ya EAC ya 1999. Tathmini fupi ya sheria hii inadokeza ukosefu wa uwazi kuhusiana na kazi ya Mamlaka za Ushuru kwenye udhibiti wa nyenzo zilizopigwa marufuku kama ilivyoamrishwa kwa nchi zote wanachama kutoka kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Dokezo hili linajaribu kuchambua kazi ya Mamlaka za Ushuru kwenye udhibiti wa mizigo iliyopigwa marufuku na Umoja wa Mataifa na ni kanuni zipi za ECA, ikiwa kuna zozote, ambazo zinahitaji kuboreshwa ili zinakiliwe na nchi zingine barani Afrika na mifumo mingine ya kieneo ya Mamlaka za Ushuru. Uboreshaji huu una uwezekano wa kuathiri, hasa kwa njia paruwanja, ufuatilizi wa bidhaa zilizopigwa marufuku za Umoja wa Mataifa, ikiwemo silaha za kawaida, bidhaa, vijenzi, au vifaa vya usambazaji, na vitu visivyoruhusiwa chini ya hatua za vikwazo vya Umoja wa Mataifa vilivyowekewa Korea Kaskazini.

2. Mfumo wa Kisheria na mapengo yaliyomo ndani

Sheria ya Usimamizi wa Mamlaka za Ushuru za Jumuiya ya Afrika Mashariki, EACCMA (toleo lililosahihishwa la 2017) inatoa msingi wa kisheria wa shuguli za mamlaka za ushuru nchini Kenya na kwenye mataifa ya Afrika Mashariki. Sheria inaidhinisha sheria maalum kwenye mfululizo mpana wa uingizaji nchini na uuzaji nje usioruhusiwa nchini. Ratiba za pili na tatu, zinaposomwa pamoja na vifungu vya 18 na 70 kwa mtawalia, zinabainisha makatazo na vizuizi hivi. Hata hivyo, sheria haitaji chochote kuhusu bidhaa/mizigo yaliyokatazwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Kimahususi zaidi, inakuja karibu zaidi kurejelea katazo la jumla kwenye ratiba ya pili sehemu A(1) miongoni mwa mengine “uingizaji nchini na bidhaa zote ambazo kwa sasa haziruhusiwi kwenye sheria hii au sheria yoyote ya kimaandishi ambayo kwa sasa inatekelezeka kwenye nchi wanachama”. Ratiba ya tatu ya sheria sawia inafafanua uuzaji nje. Mizigo iliyopigwa marufuku na Umoja wa Mataifa haikutajwa kimahususi, si uingizaji nchini, mpito, usafirishaji wa kimpito, au uuzaji nje.

Ratiba ya pili na ya tatu ya EACCMA 2017 kwa jumla huwa zinadokeza haja ya kupinga makatazo na vizuizi bila kurejelea kimahususi bidhaa/mizigo ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Inafaa kuzingatiwa kuwa nchi tofauti zina mipangilio tofauti ya kuyaidhinisha nchini Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Baadhi ya nchi zinahitaji sheria iidhinishwe, nchi zingine zinatekeleza maazimio ya Baraza la Usalama kwa amri za rais. Kivyovyote, bila kujali njia ya kuyaidhinisha nchini maazimio ya vikwazo vya Umoja wa Mataifa yawe “sheria za kimaandishi” inayozingatiwa, ni lazima kanuni zitolewe kwa idara tofauti za serikali ili sheria hizi ziweze kutekelezwa kisheria na kwa ufanisi.

Pasipokuwepo sheria ya kimaandishi inayolazimu mamlaka za ushuru zizuie bidhaa zilizopigwa marufuku na Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, inakuwa changamoto kubwa kwa nchi yoyote mwanachama kuzuia bidhaa hizo huku ikibakia ndani ya mipaka ya sheria za kimataifa.

Lakini pia kuna vipengele vya kibiashara na kiuchumi vinavyoendesha taratibu za Mamlaka za Ushuru. Maafisa wa Mamlaka za Ushuru wanashinikizwa sana wazifanyie taratibu kwa upesi bidhaa bila vizuizi rasmi visivyohitajika. Ukawiaji unaibua hatari ya kuchukuliwa hatua za kisheria na washikadau husika, ambao wanaweza kuwa watumaji bidhaa, watumiwaji bidhaa, au hata wahusika wengine. Hii inamaanisha kuwa maafisa wa Mamlaka za Ushuru wanafaa kufanya shughuli kwa upesi na makini wanapozuia bidhaa zinazoshukiwa kuwa zimekatzwa au hata bidhaa zisizoruhusiwa; lakini juu ya yote, ni lazima wafanye maamuzi sahihi kuhusiana na kuzuia bidhaa.

Hii ndiyo ilikuwa hali na ndiyo hali sasa kwa nchi nyingi za Afrika Mashariki zinaposhughulikiwa bidhaa zinazoshukiwa kuwa ni bandia. Daima huwa kuna haja ya kuhakikisha kuwa bidhaa husika zinakidhi kigezo cha kuzuiwa na kukamatwa mbeleni. Hata hivyo, kumekuwa na matendo mazuri ya kisheria ambayo yamebuniwa kuhusiana na udhibiti wa bidhaa bandia. Kwa ajili upungufu wa mamlaka za ushuru wa kushindwa kushughulikia uingizaji nchini/uuzaji nje/mpito na usafirishaji wa kimpito wa bidhaa bandia kupitia nchini Kenya, Sheria ya Kupinga Bidhaa Bandia (ACA) ilianzishwa mnamo 2008. Kifungu cha 31 cha sheria ya ACA ya 2008 inalenga hali ambapo afisa wa mamlaka ya ushuru anaweza kutenda mwenyewe (kwa kujiamulia mwenyewe) na kuwasiliana na mbebaji haki ya mali papo hapo ili kufanya uhalalishaji na uthibitishaji bila kuhofia kucheleweshe upitishaji bidhaa. Ingawa haya hayahusu vikwazo vya Umoja wa Mataifa na utekelezaji wake, juhudi na mpangilio wa kisheria uliorejelewa hapa una uwezekano mkubwa wa kuwa matendo mazuri. Pasipokuwepo kanuni wazi za bidhaa zinazohusu vikwazo vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, inakuwa ngumu zaidi kwa Mamlaka za Ushuru kutia kizuizini na/au kukamata kwa urahisi bidhaa kama hizi.

Kama ilivyofafanuliwa hapo juu, Mamlaka za Ushuru zinahitaji miongozo wazi ili ziweze kuzuia/kukamata bidhaa zilizopigwa marufuku. Ili kushughulikia bidhaa bandia, Kenya imeunda mwongozo huu wa mantiki: “mmiliki wa haki ya mali ambaye ana misingi halali ya kushuku kuwa uletaji nchini wa bidhaa bandia huenda ukatokea, anaweza kuwasilisha ombi kwa Kamishna kwa njia iliyobainishwa ili kutia kizuizini na kukamata bidhaa zote bandia zinazoshukiwa ambazo (a)… (b) Zinaletwa nchini au zinaingia nchini Kenya kwenye kipindi cha muda kilichobainishwa kwenye ombi…..” . Baada ya mazingatio na uangalifu unaoeleweka kutoka kwa Kamishna wa Mamlaka za Ushuru, mhusika, baada ya siku tatu rasmi na ikiwa ameridhishwa kimaandishi, atakubali ombi. Pasikuwepo na ombi kwa Kamishna kutoka kwa Mbebaji Haki za Mali ya Kiakili, maafisa wa Mamlaka za Ushuru (ambao pia wanafafanuliwa kama wakaguzi kwenye Sheria) wanaweza kuchukua “hatua mwafaka kwa kujiamulia wenyewe kuhusiana na matendo yoyote yanayoaminiwa au kushukiwa kuwa ni matendo yanayohusisha Bidhaa Bandia”. Huu ndio mwongozo/tiketi ya upesi ambayo inahitajiwa na maafisa wa Mamlaka za ushuru ili kuzuia na kukamata bidhaa zinazoshukiwa.

Sheria inayopatikana haitaji ni nguvu gani walizo nazo maafisa wa Mamlaka za Ushuru za kukamata mizigo/bidhaa zinazohusishwa na Korea Kaskazini kwa msingi wa katazo la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Kama vile Kenya ilivyoidhinisha sheria iliyofafanuliwa hapo juu ya kushughulikia bidhaa bandia, pia kuna haja ya kufafanua kwa uwazi miongozo ya kuzuia na kukamata bidhaa kwa Mamlaka za Ushuru kuhusiana na marufuku za Umoja wa Mataifa, hasa kuhusiana na zile zinazoelekea au zinazotoka nchini Korea Kaskazini.

3. Udhibiti wa mipaka na ukusanyaji ushuru wa mabadiliko ya kiuchumi

Mipangilio ya kisheria nchini kwenye mataifa mengi barani Afrika yanatekeleza sheria ya kudhibiti mipaka yenyewe. Mamlaka za ushuru zina kazi nne:

- Kukusanya mapato ili kuimarisha hazina ya taifa;
- Kulinda jamii (hii inajumuisha kuhakikisha kuwa mizigo/bidhaa zisizoruhusiwa haziingii nchini);
- Kurahisisha biashara ili kukuza uchumi wa taifa;
- Kukusanya takwimu za biashara – mara nyingi inatumiwa kupanga.

Matakwa haya manne yanawakilisha mfululizo mpana na mzito wa majukumu kwa viongozi wowote wa serikali moja. Kwenye Afrika Mashariki, kwa mfano, utekelezaji dhaifu wa kukusanya ushuru na uzalishaji mapato usiokuwa na mpango zimekuwa matatizo nchini Kenya, Uganda, na Tanzania, na kuchangia athari mbaya kwenye uwekezaji wa umma. Kutokana na haya, juhudi zote za Mamlaka za Ushuru zimeelekezwa tena kwenye ukusanyaji wa mapato ya nchi na ukusanyaji huu kupewa kipaumbele. Nchi nyingi zinazostawi zinapitia pamoja haja ya dharura ya kukuza mapato ya nchi huku nchi zilizoendelea zina fursa ya kudumisha makini kwenye kukuza usalama wa mipaka. Mwelekeo wa hivi karibuni wa biashara huru ulimwenguni na hatari zinazozidi kuongezeka kutoka kwa ugaidi wa kimatifa zimesababisha usalama upewe kipaumbele kwenye nchi nyingi. Hata hivyo, kiwango kinachohitajika hakijafikiwa kwa sababu anuwai.

Kwa ajili hii ndiyo hali, nchi barani Afrika zinaweza kuhitaji kuelekeza upya juhudi zao ili kulenga zaidi usalama wa mipaka badili ya lengo kuu la sasa la kukusanya mapato ya nchi. Kwa hivyo, nchi hizi zinahitaji kuunda miradi na vifaa vya pamoja vya kuhimiza mipangilio ya udhibiti ya upesi na yenye ufanisi kwenye viwango vya kitaifa na kieneo inayolenga biashara haramu inayofanywa na nchi zilizowekewa Vikwazo vya Umoja wa Mataifa. Muungano wa Afrika umejaribu mara nyingi kuzisaidia nchi ambazo ni wanachama ziendeleze sera na miongozo inayoweza kuwezesha nchi hizi wanachama zidhibiti mipaka yao vizuri zaidi. Licha ya juhudi zote hizi, nchi nyingi bado zinakumbana na changamoto za kudhibiti mipaka yao kama ilivyobainishwa na utafiti uliofanywa na Majopo ya Umoja wa Mataifa na vikundi vingine vya ufuatilizi.

Jopo la Wataalamu la Umoja wa Mataifa linaloangazia Korea Kaskazini liliripoti kuhusu shughuli zinazofanywa na kampuni za Korea Kaskazini kwenye nchi anuwai, zikiwemo Uganda, Tanzania, Uhabeshi, Msumbiji, Namibia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na Jamhuri ya Kongo. Kampuni za Korea Kaskazini zinazofanya shughuli kwenye sehemu hizi za Afrika, ikiwemo KOMID nchini Uganda au Namibia, zinakiuka vikwazo

kadhaa vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa dhidi ya biashara ya silaha za Korea Kaskazini, usafirishaji wa pesa taslimu au mbinu zingine za malipo, utoleaji kandarasi ndogo wa mafunzo anuwai ya jeshi na polisi, au ujenzi wa vituo anuwai vya serikali. KOMID na kampuni sawia za Korea Kaskazini zinaendelea kununua bidhaa kutoka Korea Kaskazini kupitia mipaka iliyo wazi na isiyolindwa kwenye eneo hilo. Mara nyingine, pia zinaingiza nchini halaiki ya wafanyakazi wa Korea Kaskazini, ambayo pia ni ukiukaji mwingine wa hatua za vikwazo vya Umoja wa Mataifa. Taasisi husika za kudhibiti mipaka zingekuwa na uwezo na ari ya kisiasa ya kuzingatia zaidi shughuli hizi, wakiukaji wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa wangekuwa wanagunduliwa, wanabainishwa, na hata pia kutiwa kizuizini kwa urahisi zaidi.

Kwa mfano Ripoti ya Wall Street Journal iliyotayarishwa na Joe Perkinson (Disemba 2018) ilidokeza jinsi, “Maafisa wawili wa kijeshi walisema kuwa waliona nyaraka zinazothibitisha ufikishaji wa silaha kutoka Korea Kaskazini hivi karibuni mnamo Agosti ambazo zilijumuisha mifumo ya kuangamiza vifaru, guruneti zinazorushwa kwa roketi, na silaha ndogo. Silaha, za vikosi maalum vya Uganda, zilisafirishwa kupitia poti ya Kenya na zikaendeshwa kwa gari usiku kucha hadi mpaka wa Kenya na Uganda, walisema.” Ripoti hii na nyingi zingine zinaonyeshwa asilia halisi ya udhibiti wa mipaka na ukosefu wa ari ya kisiasa ya kutekeleza maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Ingawa hakuna utafiti unaounga mkono dai hilo, wataalamu wa Ushuru Barani Afrika wanaamini kuwa kudumisha makini kwenye ukusanyaji wa mapato unachukua nafasi ya kuhitajika kwa dharura kwa vidhibiti vya bidhaa zisizoruhusiwa kusafirishwa kiharamu kwa kupita mipaka ya kimataifa. Kivingine, lengo kuu linaloeleweka la kukuza ukusanyaji wa mapato ya nchi linapinga haja inayoeleweka ya taifa ya kutii sheria za kimataifa – ambazo kwenye hali hii ni vikwazo vya Umoja wa Mataifa.

Hatari ya chaguo hili ni kuwa linaacha nchini nyingi barani Afrika kwenye hatari kubwa zaidi kuwa wahusika wahalifu, wanapokuwa wanakiuka vikwazo vya Umoja wa Mataifa, pia wanaweza kukiuka sheria za nchi, kuhonga maafisa, na kusababisha matatizo mengine ya usalama wa nchi. Ni lazima nafasi iliyopo ya kuboresha na kupinga ianze na kuunda miongozo wazi ya kisheria kuhusu udhibiti wa nyenzo zilizowekewa marufuku huku ikitumia uwezo wa kupata mapato yaliyokuzwa kwa njia ya faini na adhabu wakati wowote ambapo bidhaa zilizosafirishwa kiharamu zinagunduliwa au kukamatwa.

4. Mwingiliano wa kieneo na matatizo yake

Bara la Afrika lina zaidi ya mipaka 100 ya kimataifa na miongoni mwa mipaka hiyo, chini ya asilimia 35 imegawanywa wazi na kisahihi. Mipaka hii tata pia ina sifa za kiwango cha juu cha uvujaji na usimamizi mbaya. Sababu hizi zinaunda fursa za kila aina ya shughuli za kihalifu za kuvuka mipaka. Jukumu la kimsingi la kulinda mipaka ya nchi na kupigana na uhalifu ni la nchi wanachama zenyewe. Kwa hivyo, maslahi haya pacha yanafaa kuwa hamasisho ya kuimarisha udhibiti wa mipaka kwa serikali yoyote.

Nchi nyingi barani Afrika zimechagua kutatua changamoto hii pacha kwa kuunda miungano ya eneo na eneo dogo. Mfano mzuri ni Muungano wa Ushuru wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliozinduliwa na EAC mnamo 1 Julai 2014 kwenye Mamlaka Moja ya Ushuru (SCT). SCT imejengwa juu ya nguzo zifuatazo: mzunguko huria wa bidhaa, mifumo ya kusimamia mapato, mifumo ya kusimamia poti, na mpangilio wa kieneo, kisheria na kitaasisi. Uzinduzi huu uliashiria si tu utimizaji kamili wa muungano wa mamlaka za ushuru za Afrika Mashariki, bali pia unatabiri utimizaji kamili wa usafirishaji bidhaa bila malipo baina ya nchi wanachama.

Hasara iliyo wazi yenyewe ni kuwa, kwa ajili ya ukosefu wa udhibiti mwafaka wa mipaka (uvujaji wa mipaka), bidhaa sasa zinasonga kwenye eneo zima la Jumuiya ya Afrika Mashariki pindi zinapokuwa zimevuka mipaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mfano, ongezeko la hatari zilizopo za usafirishaji haramu wa nyenzo hatari kutoka Somalia hadi nchini Kenya ambazo sasa zinaweza kusonga mbele kwa urahisi hadi kwenye maeneo na vita vilivyoko kwenye nchi zingine wanachama za muungano wa kiuchumi. Kama mfululizo, inahitaji “kiungo dhaifu” kimoja tu – mipaka isiyosimamiwa vizuri – ili tatizo la nchi ligeuke na kuwa tatizo la eneo. Kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatari hizi zinaweza kuwa na athari mbaya sana. Kwa kuwa nchi zinazozunguka Jumuiya ya Afrika Mashariki ziko vitani, Somalia huko Kaskazini Mashariki, Sudani Kusini huko Kaskazini, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo huko magharibi mwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni lazima swali liulizwe kama muungano huu wa Mamlaka za Ushuru, kwenye hali mbaya kabisa, unaweza kugeuzwa na wasafirishaji haramu wa silaha uwe kituo salama cha uhamishaji haramu.

Ni kweli kabisa kuwa, faida ya kujenga muungano wa eneo ni matumaini kuwa pamoja rasilimali, ari ya kisiasa, na kushiriki upelelezi, ni kuwa utakuza usalama wa jumla mipakani. Kwa sababu hizi na sababu nyingi za kisiasa na kiuchumi, miungano ya kiuchumi ya eneo kama vile ECOWAS, SADC, au COMESA na miungano yao ya Mamlaka za Ushuru inayoendelea kubadilika, ambayo kwa upande wao inaongeza ushirikiano baina ya nchi za eneo, inawakilisha vizuri kabisa siku za usoni za udhibiti wa mipaka barani Afrika. Hata hivyo, itabakia kuwa changamoto na swali lisilokuwa na jibu iwapo mashirika haya pia yako tayari kujumuisha vikwazo na marufuku ya Umoja wa Mataifa kwenye mipangilio yake.

5. Juhudi za kitaifa za kushughulikiia changamoto za mipaka

Kumekuwa na juhudi zilizofanywa na nchi binafsi kama vile Kenya ili kushughulikia changamoto na mapengo kwenye usimamizi wa mipaka. Kenya, kwa mfano, imefuata mapendekezo muhimu ya Katibu Mkuu wa Shirika la Mamlaka za Ushuru Ulimwenguni (WCO) na nguzo zake kumi za “Mamlaka za Ushuru za Karne ya 21.” Vidokezo viwili muhimu ni:

a) Usimamizi Ulioratibiwa wa Mipaka

“Usimamizi Ulioratibiwa wa Mipaka (CBM) wa WCO unarejelea mbinu iliyoratibiwa inayotumiwa na mawakala ya kudhibiti mipaka, ya nchini na ya kimataifa, ndani ya mandhari ya kutafuta ufanisi mkubwa zaidi kwenye kusimamia biashara na mitiririko ya biashara huku inazisawazisha na mahitaji ya utiifu.” Fikra baina ya wazo hili ni kuwa, kwenye mivuko mengi ya kawaida ya ushuru, mara nyingi huwa kuna mawakala kadhaa ya serikali yanayofanya shughuli zao. Hata hivyo, kwa bahati mbaya, shughuli kwenye maghala mara nyingi huwa zinapinga ubadilishanaji wa upelelezi na maelezo muhimu sana. Kutengwa huku hakuhusishi tu mawakala ya serikali; wasimamizi wa mapato waliowekwa kwenye mivuko ya mipaka pia hawawasiliani wala hawaratibu shughuli zao.

Bila shaka, mawakala ya kudhibiti mipaka ya nchi jirani hayawasiliani na hayaratibu shughuli zao kwa sababu ya pingamizi za ziada zilizoko miongoni mwa maingiliano baina ya nchi mbili ambazo zainahitaji kiwango fulani cha itifaki.

Hata hivyo, inaonekana kuwa, kwa kiwango fulani, mawakala yote ya kudhibiti mipaka yanasaidiana kwa viwango fulani kupitia maingiliano yanayotokea baina ya watu binafasi. Kwa kuelewa thamani ya maingiliano haya muhimu baina ya binadamu kwenye kukuza usimamizi wa mipaka, pendekezo la WCO ni kuziweka sambamba kupitia maagizo ya kazi, mipango ya kuendesha shughuli, au mipangili rasmi zaidi ambayo kwa kawaida inafafanuliwa na sheria, kanuni na makubaliano.

Usimamizi Ulioratibiwa wa Mipaka, kimsingi, huwa unanuiwa kama pendekezo la kuunda uhusiano wa kikazi wenye ufanisi zaidi miongoni mwa mawakala ya kudhibiti uvukaji mipaka yaliyoko kwenye nchi sawia. Lakini, pia inapendekeza kuhusisha hatua, mipangilio, vituo sawia vya mawasiliano miongoni mwa mawakala ya kudhibiti uvukaji mipaka ya nchi jirani zenye fikra sawia.

Kuwepo kwa mawakala kadhaa kwenye vituo vya kuvuka mipaka ya nchi ni uhalisia wa mazingira ya sasa ya udhibiti ambayo hayana uwezekano mkubwa wa kubadilika

karibuni. Ingawa ni nadra kwa wakala moja pekee kuchukua jukumu la taratibu za uvukaji mipaka za nchi, mifano na vipimo vipo kote barani Afrika. Vivuko vya pamoja vya mipaka vimewekwa nchini, miongoni mwa zingine: Namanga (Mpaka wa Kenya na Tanzania) na Malaba (Mpaka wa Kenya na Uganda). Kwenye vivuko hivi vya mipaka, mawakala yote ya mipaka inaweza kufanya kazi kutoka kwenye pahali pamoja na uratibu wa kazi unatimizwa. Hakuna kizuizi halisi kinachopinga upanuzi wa taratibu zenye ufanisi za dirisha moja mipakani ili kudhibiti bidhaa haramu, zikiwemo nyenzo zilizowekewa marufuku ya Umoja wa Mataifa.

b) Udhibiti wa hatari na ufanyaji otomatiki

Mojawapo kati ya mabadiliko muhimu yaliyofanywa na mamlaka za ushuru ni kuwa nchi nyingi barani Afrika zinazifanya otomatiki taratibu zao za mamlaka za ushuru. Mifumo ya ushuru iliyofanywa otomatiki inatoa kifaa muhimu cha kuongeza uwazi kwenye tathmini ya ushuru na kodi, kupunguza kimarudufu muda wa kumaliza taratibu za ushuru, na kugundua bidhaa haramu/zisizoruhusiwa. Uanzishaji wa daraja ya juu zaidi ya ufanyaji otomatiki inaongeza uwezekano wa ukaguzi wa kina, ugunduzi wa utapeli, na hatua kali zikiwemo kufungulia mashtaka.

Uanzilishaji wa teknolojia ya hivi sasa unafaa kupewa kipaumbele na serikali za Afrika ili kupambana na uhalifu wa uvukaji mipaka. Kuna haja ya mabadiliko zaidi ya kitaasisi na upatikanaji na uidhinishaji wa teknolojia otomatiki ili kusaidia udhibiti halisi mipakani.

Mnamo 2010, kupitia mradi uliopewa usaidizi na IMF, Mamlaka ya Ushuru ya Kenya iliunda Kituo cha Kulenga cha Taifa (NTC) juu ya msingi wa NTC ya Marekani kwa mizigo na abiria. NTC ilikuwa ni ya kubobea udhibiti wa hatari kwenye Mamlaka ya Ushuru ya Kenya kama kituo kikuu cha kuainisha na kulenga mizigo yenye hatari ya kukiuka vikwazo inayoingia au kutoka nchini. NTC ilikuwa itumie mfumo wa upitishaji bidhaa wa mamlaka za ushuru wa mtandaoni unaoitwa Simba ambao tayari ulikuwa unaendeshwa (wakati huo), ambayo ilitoa udhibiti na tathmini ya hatari ya mizigo inayoingia na kutoka nchini Kenya. Simba inasaidia kung'amua kama kauli fulani ya bidhaa kwa mamlaka ya ushuru inafaa kuelekezwa kwa ukaguzi kamili, ukaguzi wa sehemu, au kama inafaa kuachiliwa iendelee na taratibu husika ya upitishaji bidhaa ya mamlaka ya ushuru bila vidhibiti vya ziada.

Mfumo imara wa udhibiti na tathmini ya hatari ni hitaji, kwa ajili ukaguzi wa kimkono wa mizigo hautosababisha uachiliaji salama na wenye ufanisi wa bidhaa ndani ya muda mfupi uwezekanao.

Ili kuweza kuonya kuhusu kushukiwa kwa nyenzo zilizowekewa marufuku za Umoja wa Mataifa, wadhibiti hatari kwenye mamlaka za ushuru wanahitaji kubuni wasifu wa hatari

wa mzigo fulani. Itabidi vigezo hivi vijumuishe, kwa kiwango cha chini kabisa, nchi ya asili ya bidhaa, ufafanuzi wa bidhaa, na kampuni inayoingiza bidhaa nchini. Haya ndiyo yanayofaa kuzingatiwa na timu ya hatari na kutekelezwa ili bidhaa zinazoshukiwa kuwa ni nyenzo zilizowekewa marufuku za Umoja wa Mataifa zinaweza kuwekewa onyo ili zifanyiwe ukaguzi wa ziada na mamlaka ya ushuru na hata kuzuiwa au kukamatwa.

Kwa ziada Mamlaka ya Ushuru ya nchi inahitaji kufuata mbinu inayotegemea hatari, yenye daraja, ya WCO ili kutekeleza sheria na kanuni zake. Hii inamaanisha kuwa, kwenye kila kiwango cha upitishaji bidhaa, maafisa wa mamlaka ya ushuru wanafaa kuwa na amri ya kutathmini hatari na kuziwekea onyo kwa mamlaka zingine ndani na nje ya mipaka ya nchi. Mkakati huu utapunguza sana hatari ya usafirishaji wa kidanganyifu wa bidhaa zinazoingia nchini, zikiwemo nyenzo zilizowekewa marufuku ya Umoja wa Mataifa.

Kuhusu Thomas Bifwoli

	Thomas Bifwoli amefanya kazi na Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Kenya (KRA); na aliidhinishwa awe Mkubwa wa Ofisi wa Ofisi ya Ushirikiano ya Upelelezi wa Kieneo ya Shirika la Ushuru Ulimwenguni ambayo ni ya Afrika Mashariki na Kusini (WCO RILO ESA). Alifanya kazi kama mratibu wa kundi la wataalamu wa ufuatilizi wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa.